Legal Aid IN PROGRESS

LSF ni Mfuko Maalum ulioanzishwa kutoa msaada wa Kifedha kwa Asasi zinazotoa msaada wa kisheria Tanzania Bara na Zanzibar.

TOLEO NA: 2
APRILI, 2013

Mwenyekiti wa ZLSC, Prof. Chris Maina, akifungua semina elekezi kwa ajili ya watu waliochaguliwa kujiunga na mafunzo ya miaka miwili ya usaidizi wa kisheria.

Mafunzo kwa wasaidizi wa sheria yaanza Z'bar

Kituo cha Huduma za Kisheria Zanzibar (ZLSC) kimeanza utekelezaji wa mradi wa kufundisha wasaidizi wa kisheria watakaoweza kuwasaidia Wanzibari kupata haki zao.

Mradi huo unafadhiliwa na Legal Services Facility (LSF), Mfuko maalum unaoyofadhiliwa na serikali ya Denmark, kwa ajili ya kutoa msaada wa kifedha kwa mashirika yanayotoa huduma za msaada wa kisheria Tanzania Bara na Zanzibar. Pamoja na ZLSC, LSF imefadhili mashirika mengine 11 10 yanayotoa msaada wa kisheria kwa ajli ya utekelezaji wa mradi wa miaka mitatu wenye malengo ya kuboresha na kupanua wigo wa huduma za kisheria nchini. Katika awamu ya pili ya mpango huu, LSF inatarajia kufadhili mashirika mengine takribani 20 yanayotoa huduma za kisheria Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa upande wake, ZLSC imeazimia kuelekeza fedha za mradi kuboresha huduma za wasaidizi wa sheria kwa kuwapatia mafunzo ya kisheria. Uandikishaji wa watu watakaojiunga na program hii ya mafunzo ya miaka miwili, ulifanyika Januari 17 Mwaka huu kwenye ofisi za ZLSC, Zanzibar, ambapo waombaji walichujwa na kati yao ni 25 tu waliofaulu.

"Tunaamini nyinyi nyote mliochaguliwa mnafaa kwa mafunzo haya...mnafaa kufanya kazi kama wasaidizi wa sheria," alisema Profesa Chris Peter Maina, Mwenyekiti wa ZLSC, ambaye pia ni mwanasheria wa haki za binadamu, wakati wa ufunguzi wa semina elekezi kwa watu waliochaguliwa kwa ajili mafunzo ya miaka miwili kwa wasaidizi wa kisheria yatayoratibiwa na ZLSC.

Chini ya mradi huu wa LSF, ZLSC inategemea kuchagua waombaji 70 kutoka majimbo 50 ya Zanzibar kwa ajili ya programu ya mafunzo ya miaka miwili--kati yao, 41 watatoka Unguja na 29 watatoka Pemba, kwa mujibu wa Bw.Jasadi Akhamad Bungala, Mratibu wa Programu wa ZLSC.

Katika mahojiano na ***Legal Aid in Progress***, mratibu huyo alisema: "Katika mchujo wa kwanza, waombaji waliofaulu ni 25 tu, wengine walishindwa kukidhi vigezo. Hata hivyo, tunatarajia kufanya uandikishaji kwa mara ya pili utakaotuwezesha kutimiza lengo letu la kupata watu 41 kutoka Unguja kwa ajili ya mafunzo haya.."

Akiongea wakati wa semina elekezi kwa waombaji waliofaulu, Mkurugenzi Mtendaji wa ZLSC, Bi. Harusi Mpatani alisema kituo kiliweka vigezo vya juu ili kupata wasaidizi wa sheria wenye uwezo "watakaosaidia watu wa Zanzibar kupata msaada wa kisheria na kurahisisha upatikanaji wa haki."

Moja ya vigezo vilivyotumiwa vinawataka wasaidizi wa sheria kutokuwa na upande wowote au kushiriki katika siasa. Kigezo hiki kina lengo la kuwafanya wasaidizi wa sheria kutoa huduma bila upendeleo wowote wa kisiasa.

"Hatutaki mtoe huduma za kisheria kwa misingi ya kisiasa kwani kwa kufanya

Endelea Uk. 2

TAHARIRI

Katika toleo hili la pili la 'Legal Aid in Progress' tuna angalia tena mchakato wa sheria ya msaada wa sheria Tanzania. Kwa maoni yetu, haya ni maendeleo muhimu ambayo yana mwekeleo wa kuweka mazingira mazuri ya huduma za msaada wa sheria nchini. Inatia moyo sana kuona kwamba serikali inafanya bidii katika ngazi za juu za kisera kuhakikisha jambo hili linatekelezwa.

Lakini hii ni habari nusu tu. Kazi nyingine kama kutayarisha mswada wa sheria na kuweka vizuri mfumo wa kisheria vinaendela vizuri na hali inaridhisha. Waandaaji na wataalamu wa sheria wanafanya kazi nzuri. Wao ni wadau wakubwa kwenye mchakato huu na ndiyo maana tunaona ni vizuri kuonesha mchango wao.

Hata hivyo, wale wanaoshiriki uandaaji wa mswada wa sheria ni vizuri wakatambua umuhimu wa wanasheria wasaidizi katika jamii. Hawa wanahitaji mafunzo ya msingi na yanayoendana na mahitaji ya walengwa. Kwa sasa mafunzo haya yanapatikana na kutekelezwa nchini. Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS) kwa msaada wa kifedha kutoka Legal Services Facility kimekubali wajibu wa kuhakikisha programu ya mafunzo inakuwa na ubora unaokubalika.

Mashirika yote yanayotoa msaada wa sheria yamekubali kwa pamoja kwamba wasaidizi wa kisheria hawana budi kuwa na elimu walau ya Kidato cha Nne, wasiwe wenye rekodi ya makosa ya jinai na wawe waadilifu wanaokubalika katika jamii. Hawa ni aina ya wasaidizi wa sheria ambao Tanzania ya leo inawahitaji zaidi kutoa huduma za kisheria kwa wananchi wa kijijini na mjini. Kutambuliwa kwao kutakuwa na matokeo mazuri kwa utoaji wa haki nchini.

Namna gani wasaidizi wa sheria wanachaguliwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) umeainishwa kwenye ibara nyingine ya 'Legal Aid in Progress'. Zanzibar ina utekelezaji wake wa kisheria tofauti. Kuna pia utaratibu tofauti wa kiutawala kuhusu msaada wa kisheria ukilinganisha na Tanzania Bara. Ukubwa wa eneo la visiwa umeruhusu kuwe na msaidizi mmoja wa sheria kwa jimbo moja (kuna majimbo ya uchaguzi 52 Zanzibar). Utekelezaji na mahitaji ya elimu ya kisheria kupitia wasaidizi wa sheria na miradi mingine ya ZLSC, unahitaji zaidi ya msaidizi mmoja wa sheria kwa jimbo moja la uchaguzi. Ili kuwezesha mpango huu, LSF inatoa msaada wa kifedha kwa ZLSC.

Msaada wa sheria unawalenga akina nani? Tunatoa mifano ya aina ya matatizo ya kisheria, ambayo wanawake kutoka sehemu mbalimbali nchini wanakutana nayo katika maisha yao. Kuna maelfu ya habari kama zinazopatikana katika toleo hili la 'Legal Aid in Progress'. Nyingi ni zile ambazo haziwezi kutafutiwa ufumbuzi unaostahili. Ndiyo maana ni muhimu kupata msaada wa sheria na inapasa uwepo mfumo mahsusi wa kisheria wa kusaidia utoaji wa msaada wa sheria na wasaidizi wa sheria.

Kees Groenendijk
Meneja Mfuko

Jarida hili hutolewa na: Legal Services Facility
Bima Street, Mikochen B Dar es Salaam, Tanzania Tel: +255 22 2781061 / +255 75 7033776
E-mail: info@lsftz.org Web: www.lsftz.org
Mhariri: Judica Tarimo

Inatoka Uk. 1

hivyo mtatoa upendeleo kwa wanachama wa chama chenu na kuwabagua wasio wa chama chenu, ambao pia wanahitaji huduma za kisheria mnazotoa," alisema Mpatani.

Kujitolea ni kigezo kingine kilichotumika kuwapata waombaji 25 waliofaulu wa kwanza, kwa mujibu wa mkurugenzi mtendaji, na kuongeza kuwa "tunawategemea nyinyi (wasaidizi wa sheria watarajiwa) kutoa huduma bila malipo yoyote."

"Tumetumia vigezo hivi kama msingi wa kuwachuja waombaji wengine, na pia tunawaonya ninyi mlichaguliwa msiombe malipo kwa wateja wenu... hawa ni watu wanaokuja na matatizo yao na wanataka wasaidiwe... wanahitaji msaada wenu," alisema mkurugenzi mkuu wa ZLSC.

Akielezea zaidi, Mpatani alisema dhana nzima ya wasaidizi wa sheria inaenda sambamba na moyo wa kujituma kutenda kazi, kujitoa na kufanya kazi kwa bidii, vitu ambavyo vilizingatiwa katika mchujo wa kuwapata wao kwa ajili ya mafunzo hayo.

"Wasaidizi wa sheria watarajiwa (walioko kwenye mafunzo)," alisema, "hawana budi kuwa waadilifu, vinginevyo watashindwa kutoa huduma zao kitaaluma. Wanahitaji pia kuonyesha moyo wa kupenda kazi na kufanya kazi kwa muda mrefu bila malipo. Haya yote tuliyazingatia wakati wa usaili," alisema.

Baada ya semina elekezi, waombaji wote waliofaulu kutoka Unguja na Pemba wataanza mafunzo rasmi ya miaka miwili yatakayowapa fursa ya kujifunza mambo ya kisheria, ikiwa ni pamoja na kufahamu Katiba ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haki za binadamu, sheri za jinai (Kanuni ya Adhabu na Sheria ya Makosa ya Jinai) na sheria nyingine.

"Tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu kuwawezesha kuzifahamu sheria ili muweze kutoa msaada wa kisheria kwa wale wenye uhitaji kwa jamii inayowazunguka," alisema Profesa Maina katika hotuba yake ya ufunguzi na kuongeza: "Ushauri wetu kwenu utaendelea hata baada ya kumaliza programu hii ya mafunzo ya miaka miwili. Lengo kuu ni kuifanya Zanzibar kuwa mahali pazuri pa kuishi."

Katika mafunzo hayo, wakurufunzi wa wasaidizi wa sheria watatoa msaada wa kisheria kwa wale wanaohitaji katika maeneo yao, kutengeneza ripoti na kuziwasilisha kituo cha ZLSC kila mwezi.

Katika ripoti zao, wakurufunzi wanatakiwa kuelezea aina za mashauri waliyoyashughulikia, idadi yake na njia zilizotumika kuyatatua. Mashauri ambayo yanahitaji utaalamu zaidi yatawasilishwa ZLSC. Wakiongea na Mwandishi wa ***Legal Aid in Progress,*** baadhi ya wakufunzi walikisifia kituo cha ZLSC kwa kuanzisha progamu hii ya mafunzo na kuahidi kutumia yale watakayojifunza kuwasaidia wananchi wanaohitaji msaada wa kisheria sehemu wanazoishi na kazini.

Rashid Hamed, Afisa Mwandamizi kutoka Taasisi ya Elimu ya Wahalifu (Institute of Education for Offenders), alisema askari magereza walio wengi wana wanyanyasa wafungwa kwa sababu ya kukosa elimu ya sheria. "Pia wako wafungwa ambao wamepoteza matumaini kwa kukosa mtu wa kuwafariji. Hivyo, programu hii ya mafunzo ya miaka miwili itaniwezesha kuwasaidia watu wa namna hii," alisema.

Abushir Said Khatibu, kutoka Jimbo la Mtoni alisema: "Kuna wanawake na watoto, ambao wana matatizo ya kisheria katika eneo langu, lakini hawajui ni wapi pa kuyapeleka ili wapate msaada. Elimu hii ya sheria itanisaidia niweze kuwasaidia katika matatizo yao."

Mtumwa Rashid Khalfan, ambaye ndiye Msimamizi wa kitengo cha maswala ya wanawake na watoto katika Tarafa ya Kiwengwe, Jimbo la Kitope, alisema: "Nimekuwa nikishugulikia kesi za wanawake na watoto kwa miaka sasa bila kuwa na elimu ya sheria na weledi. Lakini naamini kwamba baada ya kuhitimu program hii ya mafunzo ya miaka miwili, nitaweza kuyashughulikia vizuri zaidi na kitaaluma."

Ingawa Zanzibar ni ndogo kwa eneo, ndiyo sehemu yenye idadi ya wasaidizi wa sheria wengi zaidi kuliko Tanzania Bara, na kwa mujibu wa profesa Maina, hadi kumalizika kwa mradi wa ufadhili unaofanywa na LSF, idadi ya wasaidizi ya kisheria itakuwa imeongezeka.

Wadau wa sekta ya utoaji huduma za kisheria wakiwa katika picha ya pamoja katika mkutano uliandaliwa na LSF.

Waziri Mkuu aunga mkono wanaharakati

Tatizo la watu wanaohitaji msaada wa kisheria huenda likapata ufumbuzi wa kudumu baada ya baadhi ya viongozi wakuu serikalini kuunga mkono kampeni ya muda mrefu ya kitaifa kwa ajili ya kutungwa sheria ya msaada wa kisheria (Legal Aid Act).

Kwa miaka mingi sasa mashirika ya kijamii na haki ya za binadamu yamekuwa yakipigania utungwaji wa sheria ya Msaada wa Kisheria, ambayo ndiyo itakuwa suluhisho la kudumu kwa makundi ya watu maskini na wanaonyanyasika kwa sababu ya kukosa haki zao. Kwa mujibu wa ripoti za hivi karibuni zilizotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na mashirika ya kimataifa, matendo ya ukiukwaji wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na ukatili unaofanywa dhidi ya wanawake, ukeketaji, ubakaji na kulawiti, yameongezeka kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania.

Hivi karibuni, vyombo vya habari vilimkariri rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Francis Stolla akionesha kukerwa na ukiukwaji wa haki za binadamu, ikiwemo na mauji ya raia wasio na hatia yanayofanywa na jeshi la polisi (katika maeneo mbalimbali nchini) kwa kisingizio cha kulinda amani na utulivu.

Kwa mujibu wa wataalamu wa kisheria, sheria ya msaada wa kisheria (ambayo kwa sasa bado iko kwenye mchakato) inaweza kuwa msaada mkubwa kwa raia wote wanaoshindwa kupata haki hasa kwa kuzingatia kuwa wengi wao hawana uwezo kifedha.

"Ni kweli, sheria hii ikitungwa itawasaidia wananchi kupata haki, hasa maskini wasio na fedha za kulipia gharama za kuwapata mawakili na wanasheria," Juma Thomas, ambaye ni wakili wa kujitegemea na mwandishi wa habari mkongwe, alisema wakati wa mahojiano na ***Legal Aid in Progress.***

Ingawa uhusiano na umuhimu wa sheria unajulikana kwa wadau wote—serikali, kwa upande mmoja, na mashirika yanayotoa huduma za kisheria na kutetea haki za binadamu, kwa upande mwingine, juhudi zilizofanywa mpaka sasa ili kuharakisha kutungwa kwa Sheria ya Utoaji wa Msaada wa Kisheria, bado hazijaweza kuzaa matunda.

Kwa muda mrefu, mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotoa msaada wa kisheria yamekuwa yakijaribu kubuni mikakati na programu za utetezi zenye lengo la kuishinikiza serikali kutunga Sheria ya Utoaji wa Msaada wa Kisheria, lakini juhudi hizi zote zimeshingwa kutoa matokeo yaliyotarajiwa.

Hata hivyo, katika hali ya mshangao mkubwa, baadhi ya viongozi wa ngazi za juu serikalini wameanza kujitokeza hadharani na kutangaza kwamba serikali ina nia na dhamira thabiti ya kuhakikisha sheria hii, ambayo imekuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu, inatungwa na kuanza kutumika haraka iwezekanavyo.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Desemba 10 mwaka jana, Waziri Mkuu Mizengo Pinda alisema serikali ina nia ya dhati kutunga sheria ya utoaji wa msaada wa kisheria.

"Mamlaka husika ziko kwenye mchakato wa kuhakikisha sheria hii inatungwa na kuanza kutumika, ambapo naamini itawasaidia wananchi masikini kupata haki kuliko ilivyo sasa hivi," alisema Pinda.

"Tunataka wananchi, hasa walio

Endelea Uk. 4

Inatoka Uk. 3

masikini, kupata huduma za kisheria bila malipo," alisema Waziri Mkuu katika hotuba yake.

Ili kufikia lengo, alisema, serikali imeweka tayari sekretarieti ya msaada wa kisheria itakayokuwa ikiratibu huduma za msaada wa kisheria nchini.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, serikali inataka kuhakikisha kwamba utoaji wa haki unapatikana kwa wote wanaohitaji msaada wa kisheria unaotolewa na wasaidizi wa kisheria.

"Ili kupata haki na kuongeza ufanisi katika utoaji haki, serikali imeanzisha programu ya kuajiri wanasheria katika mahakama za mwanzo ili kusaidia kukabiliana na ucheleweshaji na uvunjaji wa haki za binadamu," alisema Pinda.

Kwenye hotuba yake wakati wa uzinduzi wa Sekretarieti ya Msaada wa Kisheria mwaka jana, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Angela Kairuki, alisema utoaji wa huduma za kisheria bila malipo ni muhimu sana katika upatikanaji wa haki Tanzania.

"Ni moja ya mambo ya msingi katika kupata haki, ambayo hatuna budi kuyatekeleza kama tunataka haki sawa mbele ya sheria na usawa katika upatikanaji wa haki kwa wote," alisema.

Alizungumzia pia nia ya serikali kuunga mkono kwa moyo wote mchakato wa utungaji wa Sheria ya Msaada wa Sheria.

Kauli ya Waziri Mkuu, kwa upande mmoja, na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, kwa upande mwingine, zinaonesha moyo wa thabiti wa serikali katika kuwasaidia watu maskini kupata haki.

Tike Mwambipile, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), aliona matamko yao kama hatua kubwa katika kampeni ya muda mrefu ya kuisukuma serikali kutekeleza wajibu wake wa kutoa na kusaidia upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi wa kawaida.

Kwa miaka mingi sasa, kazi ya utoaji wa msaada wa kisheria imeachwa mikononi mwa mashirika yasiyo ya kiserikali, lakini mara tu sheria mpya itakapoanza kutumika, serikali itarejea wajibu wake wa kutoa na kusaidia utoaji wa msaada wa kisheria bila malipo kwa watu wanaohitaji, kwa mujibu wa Mwambipile.

Ingawa kuna juhudi za kutunga sheria, kupata haki na msaada wa kisheria bado ni tatizo kubwa Tanzania. Kwa mujibu wa repoti ya 2011 kuhusu upatikanaji wa haki na msaada wa kisheria Afrika Mashariki – uchunguzi wa kifani kutoka Tanzania, Kenya na Uganda, umebaini kuwa bado kuna changamoto nyingi kuhusu utoaji wa haki Tanzania, ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji wa kesi mahakamani.

Ripoti iliyotayarishwa na Taasisi ya Kidenishi ya Haki za Binadamu ilionesha kwamba "tatizo linasababishwa na Tanzania kutokuwa na wanasheria wa kutosha waliobobea, hasa katika sekta ya umma."

Ripoti pia inaonyesha matatizo mengine yanayoathiri upatikanaji wa haki, kama vile ukosefu wa sera na sheria zinazohakikisha msaada wa kisheria unatolewa katika kesi za jinai na madai vijijini na mijini.

Hata hivyo, kwa kipindi fulani, Mheshimiwa Angela Kairuki alinukuliwa na ripoti maalumu akielezea uanzishaji wa vyombo viwili —sekretarieti ya msaada wa kisheria iliyoanzishwa na serikali ya Tanzania na Mfuko maalum wa LSF unaofadhiliwa na serikali ya Denmark—kama mafanikio makubwa katika mchakato mzima wa kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote, hasa kwa masikini na makundi ya watu wa pembezoni."

Tayari, LSF, imetoa shilingi zaidi ya bilioni 4 pesa za kitanzania kwa mashirika 12 yanayoto huduma za sheria (makubwa na madogo) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa miaka mitatu, ambao wataalamu wamesema utakuwa na matokeo chanya katika swala zima la upatikanaji wa haki hapa nchini. Mwaka 2013, LSF itafadhili pia mashirika mengine yanayotoa msaada wa kisheria.

Katika mahojiano ya hivi karibuni na gazeti la kila siku la Kiingereza, ***The Guardian***, Christina Kamili, Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Utoaji wa Huduma za Kisheria Tanzania (TANLAP), alipendekeza kuwepo kwa ibara katika Katiba mpya itakayohakikisha raia wote wanapata haki ya kupata msaada wa kisheria bila malipo na uwakilishi mahakamani.

UCHANGANUZI

Mchakato kuelekea Sheria ya Msaada wa Kisheria

Na Daniel N. Lema (Mratibu Sekreterieti ya Msaada wa Sheria)

Wasaidizi wa kisheria wakijadiliana katika mkutano uliofanyika Dodoma.

Utangulizi

Katika toleo la kwanza, chapisho Na.1 la 2012, niliandika makala inayofanana na hii kwa karibu yenye kichwa cha habari ***"Hatua kubwa kuelekea kupata haki sawa kwa wote".*** Makala hii ilielezea masuala mbalimbali yanayohusiana na urasmi wa huduma za kisheria Tanzania na mchakato unazoendelea wa utungaji wa sheria (Legal Aid Act) ambayo itasimamia utoaji wa huduma za msaada wa kisheria nchini.

Ninafurahi kusema kwamba mafanikio makubwa yameshaanza kuonekana katika mchakato mzima wa kutunga sheria hii—pongezi kwa kazi nzuri ya Wizara ya Katiba na Sheria na Kikosi kazi kilichoundwa na serikali kusimamia mchakato mzima wa utungaji wa sheria husika. Makala hii ya pili itaonesha maendeleo ambayo yamepatikana katika mchakato nzima wa kutunga sheria hii, na kuondoa baadhi ya mashaka na kujibu maswali juu ya utekelezaji wa sheria husika.

Maendeleo ya uandikaji wa ripoti

Awali ya yote, sina budi kuwashukuru wajumbe wa Kikosi kazi kwa kazi kubwa waliyoifanya mpaka sasa. Wakiongozwa na moyo huu wa kujitoa, wameweza kuja na rasimu ya ripoti kuhusu utungaji wa sheria ya Msaada wa Kisheria Tanzania. Waraka huu ulisambazwa kwa mara ya kwanza kwenye mkutano wa wadau ulioitishwa (hivi karibuni) kimkakati kwa ajili ya kukusanya maoni ya wadau ili kuboresha ripoti kuhusu muswada wa sheria.

Kimsingi, muswada huu ulipendekezwa uwe na sehemu saba zitakazohusu masuala mbalimbali ya utoaji wa msaada wa kisheria. Nazo ni **Mambo ya awali**, **Uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi na Shughuli Zake, Secretarieti ya Mamlaka, Fedha, Utoaji wa Msaada wa Kisheria, Usimamizi wa Mashirika Yanayotoa Msaada wa Kisheria na Mambo mbalimbali.** Kila sehemu ya sheria hii inaendana na mahitaji ya watoa huduma za msaada wa sheria na wadau.

Lakini kuandaa ripoti ya muswada haikuwa kazi rahisi—ilitokana na utafiti uliofanywa mwaka jana na ziara ya wajumbe wa Kikosi kazi. Wajumbe walitembelea nchi tatu za Afrika ambazo ni Malawi, Zambia and Uganda. Nchi hizi zina mifano hai ya huduma ya msaada wa kisheria. Lengo kuu la ziara lilikuwa kujifunza ni namna gani huduma hizi zinaweza kutolewa kwa ufanisi zaidi. Moja ya hadidu za rejea ilikuwa ni kuona ni kwa namna gani wasaidizi wa sheria wanatoa huduma za msaada wa sheria katika nchi hizo.

Kwa kweli, wajumbe walijifunza mambo mengi na baadhi ya yale waliyojifunza yameingizwa kwenye rasimu ya muswada wa sheria kuhusu utoaji huduma za msaada wa kisheria. Mambo hayo ni pamoja na uwepo wa vyombo vinavyosimamia msaada wa kisheria, uwepo na utambuzi wa wasaidizi wa sheria, ushiriki wa mashirika ya kijamii katika utoaji wa msaada wa kisheria na chombo cha serikali kinachofadhili utoaji wa huduma za msaada wa kisheria.

Kinyume na matarajio ya kikosi kazi, katika nchi zote hizi wasaidizi wa sheria hawawakilishi wateja wao mahakamani au kwenye mabaraza. Kwa kifupi, haya ni baadhi ya mafunzo muhimu yaliyopatikana na yamesaidia katika uandaaji wa rasimu ya muswada wa sheria husika.

Jukwaa la wadau na changamoto zake

Kama nilivyosema hapo juu, baada ya michakato miwili – utafiti wa kutembelea nchi nyingi na rasimu ya muswada wa sheria, kikosi kazi kiliandaa jukwaa la wadau wote katika utoaji wa msaada wa kisheria, wakiwemo na wale ambao wanashiriki moja kwa moja katika utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria. Kwa ujumla, wadau walikipongeza Kikosi kazi kwa kujituma na kazi nzuri waliyofanya, na hatimaye kujadili kwa kirefu baadhi ya masuala muhimu ambayo yanatakiwa yazingatiwe kabla ya kuyaingiza katika rasimu ya muswada wa sheria. Masuala hayo ni hasa sifa za wasaidizi wa sheria na uwakilishi.

Ripoti ya rasimu inapendekeza kwamba kwa mtu yeyote kukubaliwa kuwa msaidizi wa sheria anatakiwa awe amefanya mafunzo yaliyoidhinishwa na mamlaka ya msaada wa sheria itakayoanzishwa na sheria hii, ikiwa ni pamoja na kuwa mwadilifu. Ripoti ya rasimu ya muswada wa sheria ulipendekeza vigezo kadhaa vya kuangalia ili mtu awe msaidizi wa sheria – digrii ya kwanza na uzoefu usiopungua miaka mitatu, diploma katika sheria au masomo yanayohusu usadizi wa sheria na uzoefu usiopungua miaka miwili katika kazi ya usaidizi wa sheria na cheti katika sheria na uzoefu usiopungua miaka minne katika kazi ya usaidizi wa sheria.

Hata hivyo, vigezo vilivyotajwa hapo juu (kwa kutambua na kuwakubali wasaidizi wa sheria) vimeibua gumzo miongoni mwa wadau wakisema vigezo viko juu sana, ambavyo ni wachache tu wataweza kukidhi viwango hivyo. Mambo yaliyoibuliwa na wadau ni kwamba wasaidizi wa sheria walio wengi katika mfumo wa sasa hawataweza kukidhi vigezo vilivyopendekezwa kwenye ripoti hiyo.

Haya ni baadhi tu ya mambo ambayo wadau wa sheria waliyasema wakati wa mkutano uliolenga kukusanya maoni juu ya rasimu ya muswada wa sheria ya huduma za sheria. Hata hivyo, ilikubaliwa kwamba mamlaka husika ipewe jukumu la kuwathibitisha, kuwatambua na kuwakubali wasaidizi wa sheria kwa kuzingatia dukuduku zilizotolewa na wadau—kwa kutafuta njia ya kati (middle ground) ambayo haitaathiri upatikanaji wa wasaidizi wa sheria wenye weledi na wakati huohuo haitawaondoa wasaidizi wa sheria ambao wamepata mafunzo na uzoefu kwa muda mrefu na wanafanyakazi hiyo kwa sasa.

Turn to Page 6

From Page 5

Mamlaka ya uthibiti na mashaka ya wadau

Jambo lingine linahusu shughuli za mamlaka inayosimamia shuguli za utoaji wa msaada wa sheria. Kuna mashaka kwamba mamlaka ya msaada wa sheria iliyopendekezwa kuundwa na sheria mpya, inaweza kurudia shughuli ambazo zinafanywa na baadhi ya vyombo vya serikali. Kwa kuzingatia ukweli kwamba kuna Mkurugenzi katika Wizara ya Katiba na Sheria inayosimamia shughuli za utoaji wa msaada wa kisheria. Pia kuna minongo'no kuwa sekretarieti ya msaada wa sheria itakuwa pia ikifanya shughuli za mamlaka ya kusimamia shughuli za utoaji huduma za kisheria iliyopendekezwa katika sheria mpya.

Ijulikane kwamba hata baada ya uanzishwaji wa mamlaka ya msaada wa sheria, Kurugenzi ya Huduma za Kisheria za Umma (PLSD) kwenye wizara itaendelea kufanya kazi—ikijikita zaidi katika maswala ya sheria na miuongozo mingine, wakati mamlaka mpya ya kusimamia utoaji wa huduma za sheria itafanya kazi kama chombo cha usimamizi/uthibiti wa huduma za kisheria. Hivyo, vyombo hivi viwili (PLSD) na mamlaka ya kusimamia utoaji wa huduma za sheria) vitakuwepo na vitakuwa na shughuli tofauti.

Ni lazima watu waelewe pia, sekretarieti ya msaada wa sheria ni "kiungo" kinachowaunganisha watoa huduma za sheria kwa sasa, na ni "daraja" linalounganisha serikali na watoa huduma za sheria katika mchakato mzima wa kutafuta chombo cha kudhibiti utoaji wa msaada wa sheria Tanzania. Mara baada ya mamlaka ya sheria kuanzishwa, sekretarieti ya msaada wa sheria "itakufa" na kazi zote zitakuwa zinafanywa na mamlaka ya utoaji wa huduma za kisheria.

Naamini maelezo haya yamesaidia kuweka mambo sawa na kuondoa wasiwasi na mashaka ya wadau.

Tunakoelekea

Baada ya kukusanya maoni ya wadau, Kikosi kazi kinategemea kuwasilisha wizarani ripoti inayohusha rasimu ya muswada wa kutunga sheria ya msaada wa sheria Tanzania. Wizara itaandaa nyaraka mahsusi kuhusu dhana nzima ya sheria husika na kuziwasilisha kwenye kamati ya kiufundi (IMTC) inayowahusisha makatibu wakuu wote kwa ajili ya kufanya mapitio, kufanya mapendekezo na mambo mengine yanayoendana na hayo.

Baada ya kuridhika na rasimu ya msaada wa sheria, kamati itapeleka nyaraka kwenye Baraza la Mawaziri kupata idhini ya kuundaa muswada wa sheria husika.

Baada ya kuridhika, Baraza la Mawaziri litaridhia rasimu ya muswada wa sheria. Mchakato bado unaendelea. Kwa hatua hii serikali inastahili pongezi kwa kuonesha nia ya dhati ya kutunga sheria ya Msaada wa Sheria.

Hitimisho

Kama kila kitu kitaenda kama kilivyopangwa, Tanzania itakuwa, kwa mara ya kwanza, na Sheria ya Msaada wa Sheria kabla ya mwisho wa mwaka huu. Ni matarajio ya wananchi na wadau wengi kuwa sheria hii itakuwa mkombozi kwa watu masikini kupata haki sawa na fursa ya kupata wawakilishi wa sheria mahakamani.

Wahanga walonga

Vitisho katika Ndoa...

Jina langu ni Honoratta Duttilo. Mume wangu ana umri wa miaka 60 na anafanya kazi kama injinia kwenye Kambi ya Jeshi Mzinga iliyopo Mkoa wa Morogoro. Mimi ni Mkristo na mume wangu ni Mwislamu. Kutokana na tofauti za kiimani, tulikubaliana kufunga ndoa ya kiserikali na kupata cheti kinachoonesha ndoa yetu ni ya mume na mke mmoja.

Tulifunga ndoa Januari 28, 1989 na tumejaliwa watoto wanne. Tumeishi pamoja kwa amani kwa miaka mingi. Mwaka 1991, tulipata kiwanja Wilaya ya Chamwino na kujenga nyumba yenye vyumba vinane. Tuliishi kwa kupendana na tulifurahia ndoa yetu.

Hata hivyo, miaka michache iliyopita, matatizo yalianza kujitokeza kwenye ndoa yetu—mume wangu alianza kunichukia bila sababu ya msingi. Matatizo yalianza kidogo kidogo, lakini yalianza kukua siku hata siku. Ghafla alikataa kulipa ada ya watoto shuleni na kuacha fedha za chakula nyumbani kama alivyokuwa akifanya hapo awali. Pamoja na hayo, alianza kurudi nyumbani kwa kuchelewa sana kila siku. Kwa kweli nilijiuliza maswali mengi ni kitu gani kimembadilisha mume wangu lakini sikupata jibu.

Bi. Honoratta Duttilo (Kushoto), akieleza matatizo yake wakati wa mahojiano maalumu na Mhariri wa Kijarida cha Legal Aid in Progress, Judica Tarimo, yaliyofanyika Mjini Morogoro.

Ni kama alikuwa ameacha familia. Alianza kuwa ananitukana na kunipiga mbele ya majirani na wapita njia.

Nikiwa mke wa nyumbani, sikuwa na la kufanya. Nilihitaji fedha kwa ajili ya kuwalisha watoto wangu, kulipa ada ya shule na mahitaji mengine muhimu. Tulipata matatizo ya kifedha yaliyoathiri zaidi watoto wangu na mimi mwenyewe.

Hivyo, nilianza kutafuta msaada serikali za mitaa na ofisi za ustawi wa jamii, lakini sikufanikiwa kwani matatizo yalizidi kuongezeka. Baada ya muda, uongozi wa Chuo cha Ufundi cha Veta Morogoro ulitaka kuwafukuza watoto wangu kwa kushindwa kulipa ada ya shilingi 30,000. Nilienda kwa mjumbe Magreth Mbilizi pale Kihonda. Alituita mimi na mume wangu na tukashauriana, lakini hatukupata suluhisho. Niliamua

Turn to Page 7

Inatoka Uk. 6

kufanya kazi ya kubeba matofali kichwani kwa ajili ya kupata shilingi 30,000 za kulipa Veta.

Cha kushangaza, mume wangu alikasirika na kwenda kunishtaki kwa mjumbe akisema: "Nilikuwa nafanya kazi iliyomwaibisha yeye kama injinia wa kambi ya jeshi." Mjumbe alituasa kujadiliana na kupata suluhisho. Kwa upande mwingine hakutendea haki kwa sababu alianza kunilaumu mimi kwa kumkosea heshima mume wangu mbele ya jamii. Kwa mara nyingine tena, mume wangu alikataa kulipa ada ya shule na kutunza familia.

Lakini siku moja nilisikia tangazo kwenye radio kuhusu msaada wa kisheria unaotolewa na Kituo cha Wasaidizi wa Sheria cha Morogoro. Siku iliyofuata nilienda kituoni hapo kuomba msaada wa kisheria. Nilikutana na Bi. Flora Masoy, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho.

Kwa ushirikiano na wafanyakazi wengine wa kituo, Bi. Masoy alinipa ushauri nasaha. Tulijadiliana kuhusu hili suala langu kwa undani zaidi na mume wangu alisaidiwa kuelewa kwamba ndoa yetu ilikuwa ya mume na mke mmoja. Hatimaye, tulifikia mwafaka kwamba mume wangu awe ananipa shilingi 100,000 kila mwezi kwa ajili ya matunzo ya familia. Iliamuriwa kwamba nitapewa fedha hizo kupitia kituo cha msaada wa sheria na nitazichukua kutoka hapo. Ninafurahi kusema kwamba miezi mitatu imepita na tangu nianze kupokea shilingi 100,000—walau naweza sasa kununua chakula na kutunza familia.

Mjane anyimwa haki yake ya urithi

Maria John (miaka 50) alifunga ndoa ya kimila na Maulid Salehe Kitogo mwaka 1991. Mume alikuwa ameajiriwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Miaka minne baada ya kuishi pamoja kama mume na mke, walipata mtoto wao wa kwanza Salehe Kitogo mwaka 1994, muda ambao walijenga nyumba Mtoni-Kichangani, Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam. Mtoto alilelewa na wazazi wote wawili.

Kwa bahati mbaya, mwezi Desemba 1999, mume aliugua. Ndugu na jamaa kutoka pande zote mbili walikutana kujadili nini kifanyike na hatimaye waliamua kumrudisha kijijini kwao huko Morogoro ili ajaribu tiba ya dawa mbadala.

Maria John, mjane akieleza mkasa uliompata Bi. Catherine Madili, mmoja wa maafisa wa Kituo cha Wasaidizi wa Kisheria kilichopo Wilaya ya Temeke.

…Wanawake ambao wamekuwa wakinyanyasika kijinsia wamesaidiwa na mashirika yanayotoa msaada wa kisheria yanayofadhiliwa na LSF

Hata hivyo, haikusaidia kitu na afya yake iliendelea kuzorota na hatimaye kufariki dunia Novemba 2011.

Ndugu wa mume walivamia nyumba ya marehemu na kumfukuza mjane kwenye nyumba hiyo. Wakiongozwa na kaka wa marehemu, ndugu hao walidai mke hana haki ya kurithi nyumba na mali nyingine.

Kutokana na kukosa maelewano, mwaka 2009 mjane aliamua kufungua kesi ya mirathi Mahakama ya Mwanzo ya ya Temeke. Hukumu ya kesi ilitolewa Julai 8, 2009 na kumpa mjane haki ya kuwa msimamizi wa mirathi katika ukusanyaji na ugawanyaji wa mali yao. Kwa kutoridhishwa na hukumu iliyotolewa, ndugu wa marehemu waliamua kufungua kesi nyingine ya madai Mahakama ya Mwanzo Magomeni kupitia mlango wa nyuma bila kumshirikisha mjane.

"Walishinda kesi, lakini sikuwa na taarifa yoyote kuhusu kesi hii… Mahakama haikuniita ili kusikia upande wangu. Ndugu wa marehemu walikuja na barua kutoka mahakamani, ikinitaka nitoke pale nyumbani. Nilienda mahakamani hapo na kutoa vielelezo vikionesha kesi hii ilikuwa imeshaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Temeke," alisema.

"Kwa kuchukizwa na mbinu chafu za kufungua kesi kinyume cha taratibu, Mahakama ya Mwanzo Magomani ilisimamisha mchakato wa urithi. Hivyo, ndugu wa marehemu waliamua kukata rufaa kwenye Mahakama ya Wilaya Temeke," alieleza mjane.

Wakati kesi ikiwa inaendelea kwenye mahakama hiyo ya wilaya, mjane alifungua kesi ya jinai katika mahakama hiyohiyo dhidi ya ndugu wa marehemu kwa kukataa kutoa hundi hundi ya marehemu na hati miliki ya nyumba.

"Hivyo, tulikuwa na kesi mbili kwenye mahakama moja," alisema Maria wakati wa mahojiano na ***Legal Aid in Progress.***

"Nilijiuliza, nifanye nini? Nitawezaje kukabiliana na hizi changamoto za kisheria? Wakati huo nilikuwa sina fedha," alielezea. Kwa bahati nzuri, mtu mmoja alinishauri nitafute msaada wa kisheria kutoka kituo cha msaada wa kisheria karibu kilicho chini ya Kituo cha Ustawi wa Wanawake na Watoto Tanzania Women (TWCWC).

Wanasheria na wanasheria wasaidizi walimsaidia mjane kuandaa nyaraka za kimahakama kwa muda wote wa kesi na Oktoba 2010 hukumu ilitolewa na kumpa mjane haki.

"Kituo cha msaada wa sheria kilinisaidia bila malipo yoyote hadi niliposhinda keshi. Nina kishukuru sana kituo hiki… hawa watu ni wakarimu na wanajitoa sana. Sijaweza kuona na kupata uzoefu wa watu kama hawa maishani kwangu," alihitimisha mjane.

Mashirika yanayofadhiliwa na LSF yanafanya kazi gani?

Wito wa kwanza wa mapendekezo ulizinduliwa Mei 17, 2012. Wito huu ulipelekea mashirika 12 yanayotoa msaada wa sheria kuingia mkataba kama wafadhiliwa.

Mashirika 10 yanayofadhiliwa yanashirikisha jumla ya wilaya 64 ambazo mwanzoni hazikuwa na huduma za msaada wa sheria.

Utafiti uliofanywa na LSF unaonesha kwamba takriban wilaya 50 zilikuwa na aina fulani ya msaada wa sheria. Kwa hiyo, kupitia wito wa kwanza wa mapendekezo, kumekuwa na ongezeko la sehemu za kutoa msaada wa sheria kwa asilimia 125. Kwa vile Tanzania ina wilaya zipatazo 148 kwa sasa (ambazo zinaweza kuongezeka) hii ina maana kwamba bado kuna wilaya takriban 34 ambazo hazijafikiwa na huduma za msaada wa sheria ili kufanya wilaya zote ziweze kufikiwa nchini.

Kwa kuongezea, Chama cha Wanasheria Tanganyika, kimekubali wajibu wa kushughulikia maudhui ya kitabu cha mwongozo wa mafunzo ya wasaidizi wa sheria na mafunzo ya wasaidizi wa sheria. Hiki ni kiungo muhimu katika utoaji wa huduma zenye ubora kwa jamii.

Shirika la Mazingira, Haki za Binadamu na Jinsia (Envirocare) limekubali wajibu mwingine katika utoaji wa huduma za sheria. Envirocare itafanya kazi katika magereza 24 katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro na Manyara. Katika magereza haya walengwa ni wale waliowekwa kizuizini wakati wakisubiri kesi zao kusikilizwa na kuamriwa. Katika magereza yote nchini, asilimia 55 ya watuhumiwa wote ni wa kesi za rumande, ambao huenda wameshtakiwa kwa kutenda makosa madogo madogo. Mtu aliye kizuizini anaweza kukaa gerezani kwa miaka kadhaa na mara nyingi anaweza kukaa muda mrefu zaidi ya kiwango cha juu kutokana na kosa alilolitenda (ingawa hii inabidi ithibitishwe kwani mtu aliye kizuizini ni mshtakiwa tu). Huu ni ukiukwaji wa haki za binadamu unaosababishwa na uzembe katika mfumo wa utoaji haki kwa makosa ya jinai. Kwa mara ya kwanza tatizo hili limetafutiwa ufumbuzi Tanzania.

Mashirika yaliyofadhiliwa na kiasi cha fedha

Jina La Shirika	Kiasi cha Fedha Kilichopokewa (Tshs)	Jina La Mradi
Wanaweke Amkeni (WOWAP)	240,000,000	Kuongeza Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake na Watoto Magerezani na Katika Jamii
Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC)	694,831,250	Kuongeza Msaada wa Sheria kwa Watu wengi Zaidi
Shirika la Wanawake la Kubadilishana Habari na Ushauri Kilimanjaro (KWIECO)	719,990,000	Kuongeza Upatikanaji na Kujenga Uwezo wa Utoaji wa Msaada wa Sheria Katika Wilaya Sita za Mkoa wa Kilimanjaro
Utendaji Haki Katika Jamii (AJISO)	232,072,880	Kuongeza Msaada wa Sheria ili Kupata haki za Kijamii
Shirika la Msaada wa Sheria la Matumaini ya Mama (MHOLA)	239,998,198	Kupeleka Huduma ya Msaada wa Sheria Karibu na Jamii
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)	720,000,000	Kuongeza na Kuboresha Upatikanaji wa Haki kwa Maskini
Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC)	720,000,000	Msaada wa Sheria na Programu ya Kupandisha Hadhi Huduma za Msaada wa Sheria
Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA)	720,000,000	Upatikanaji wa Haki Kupitia Uanzishwaji wa Mtandao wa Wasaidizi wa Sheria katika Wilaya 11
Chama cha Sheria Tanganyika (TLS)	480,000,000	Kukuza na Kuendeleza Vitabu vya Mwongozo wa Mafunzo ya Watoa Msaada wa Sheria
Kituo cha Ustawi wa Wanawake na Watoto (TWCWC)	239,819,355	Kukuza Upatikanaji na Huduma za Msaada wa Sheria kwa Ngazi ya Wadi
Shirika la Mazingira, Haki za Binadamu na Jinsia (ENVIROCARE)	719,999,790	Mahabusi na Walio Kizuizini Tanzania
Kituo cha Msaada kwa Wajane na Watoto (CWCA)	239,997,790	Kukuza Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake Maskini na Watoto kupitia Wasaidizi wa Sheria